# OFISI YA WAZIRI MKUU
# SERA BUNGE NA URATIBU

JARIDA LA MTANDAONI: www.pmo.go.tz | DODOMA | TOLEO LA AGOSTI 2022



KATIBU MKUU OFISI
OFISI YA WAZIRI MKUU SERA BUNGE NA URATIBU
2 BARABARA YA POSTA 40412 DODOMA TANZANIA

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa



# Waziri Simbachawene: kazi ndio heshima ya mtu

Wakristo nchini wametakiwa kufanya kazi kwa bidii ili kujietea maendeleo, changia pato la Taifa na kutatua changamoto zilizo katika maeneo yao

Hayo yameelezwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Mhe. George Simbachawene wakati akizunguma katika sherehe ya kumweka wakfu Askofu wa tatu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Mpwapwa, Rev. George Chiteto iliyofanyika Jijini Dodoma baada ya aliyekuwa askofu wa kanisa hilo Askofu Donald Mtetemela kumaliza muda wake ..

Waziri Simbachawene alisema chanamoto nyngi za kiuchumi katika jamii zitatauliwa endapo wananchi watajituma kufanya kazi na kuwa wabunifu kwa kuanzisha miradi mbalimbali kama ambavyo maandiko matakatifu yanaagiza watu kufanya kazi.

“Lazima wakristo wa sasa tufanye kazi lazima tutae changamoto kwenye maeneo yetu maana imeandikwa katika biblia asiyefanya kazi na asile kwahiyo kufanya kazi ndio uhai wako, heshima yako na ukizalisha utaweza kuendesha maisha yako binfasi, utashiriki katika kazi ya Mungu na Taifa zima,” alisema Waziri Simbachawene.

ushirikiano na taasisi za dini kwani zimekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo, kusimamia maadili na kupambana na vitendo vya mmomonyoko wa maadili kwa baadhi ya watu wasiyo na hofu ya Mungu.

"Licha ya mchango mkubwa wa kanisa hili kwa serikali lakini kumekuwa na mmomonyoko wa maadili, magonjwa na majanga mbalimbali hivyo ni muhimu kushirikiana na serikali ili kuokoa vijana na watoto wetu na ni matumaini yetu viongozi wa dini mkiendelea kusimama imara na kutoa huduma ya kiroho tutatatua changamoto hii," alieleza.

Pia aliongeza kwamba serikalii itaendelea kushirikiana na taasisi za dini kwani zimekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo, kusimamia maadili na kupambana na vitendo vya mmomonyoko wa maadili kwa baadhi ya watu wasiyo na hofu ya Mungu.

"Licha ya mchango mkubwa wa kanisa hili kwa serikali lakini kumekuwa na mmomonyoko wa maadili, magonjwa na majanga mbalimbali hivyo ni muhimu kushirikiana na serikali ili kuokoa vijana na watoto wetu na ni matumaini yetu viongozi wa dini mkiendelea kusimama imara na kutoa huduma ya kiroho tutatatua changamoto hii," alieleza.

Aidha alibainisha kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan imeendelea kuchukua hatua za kisheria kwa watu wote wanaojihusisha na vitendo vya rushwa , ufisadi, utovu wa nidhamu kwa watumishi wa umma pamoja na jamii kwa ujumla.

Kwa upande wake Askofu Mkuu wa Kanisa Anglikana Tanzania Mhashamu Dr. Maimbo Mndolwa aliipongeza serikali kwa kuwa mstari wa mbele kuziunga mkono taasisi za dini katika nyanja zote huku akimtaka Askofu Chiteto kufanya kazi kwa kumtegemea Mungu hatimaye kufikia malengo ya kanisa.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule alitoa wito kwa wakazi wa mkoa huo kutumia fursa ya serikali kushusha bei ya mbolea kwa kujikita katika kilimo.

Waziri Simbachawene: kazi ndio heshima ya mtu



## Jitokezeni kwenye zoezi la sensa ili muhesabiwe

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu Mhe. George Simbachawene amehimiza wananchi kujitokeza kuhesabiwa katika zoezi la sensa ya watu na makazi kwa ajili ya maendeleo yetu wenyewe.

“Unapohesabiwa unakuwa upo katika mpango wako wa maendeleo, katika sehemu yako unayoishi na Nchi kwa ujumla” Hayo yamesemwa na waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu Mhe. George Simbachawene baada ya kushiriki zoezi la sensa ya watu na makazi jimboni kwake Kibakwe katika Halmashauri ya

Amefafanua kwamba usipohesabiwa, unakosa lile fungu lako katika miaka 10 ijayo kwa ajili ya mipango ya maendeleo.

“Bado tuna siku tano mbele kwa ajili ya kuhesabiwa hakikisha umeacha kumbukumbu za watu walilolala usiku wa kuamkia tarehe 23 Agusti 2022, alisema Waziri”



# Watendaji wahimizwa kuongeza kasi utekelezaji wa Mradi wa AFDP

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu Mhe. George Simbachawene amehimiza kuwa na vikao vya uratibu vya pamoja kati ya wizara na taasisi zinazotekeleza mradi wa mradi wa AFDP ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi.

Hayo yamesemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu Mhe. George Simbachawene alipotembelea shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) Kigamboni Jijini Dar es salaam ambalo linatekeleza programu ya kuendeleza kilimo na uvuvi katika mradi wa AFDP unaoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu sera Bunge na Uratibu na kutekelezwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi – Zanzibar.

Waziri Smbachawene amesema programu AFDP ni ya miaka sita kuanzia 2021/2022 hadi 2027/2028 ambayo itagharimu jumla ya Dola za Kimarekani 77.4 millioni (Mkopo toka IFAD USD 58.8 millioni; Serikali USD 7.7 millioni; Sekta Binafsi 8.4 millioni na Wananchi USD 2.4 millioni).

"Mradi huu wa uchumi wa bluu ukisimamiwa vizuri utaibua shirikia la TAFICO, na utaibua uchumi wa biashara ya uvuvi zinazofanywa na sekta binafsi. "

Lazima tutengeneze kikosi kazi kitakachokuwa kinaashughulikia changamoto zinazojitokeza kutoka taasisi moja kwenda nyingine pamoja na wizara moja kwenda nyingine katika utekelezaji wa mradi, alisema Waziri.

"Eneo hili linaloshughulikiwa na shirika la TAFICO linaenda kujibu ahadi za ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020-2025."

Naye Katibu Mkuu Ofisi ya waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu Dkt. John Jingu amesema mradi huu ni mradi mkubwa sana na ni mradi wa kimkakati.

"Tuone namna ambavyo tutautekeleza huu mradi kikamilifu, spidi na kasi ya utekelezaji wa mradi bado hairidhishi."Kwa upande wake Mwenyekiti wa bodi ya shirika la TAFICO Profesa Yunus Mgaya amesema wanalichukulia shirika la TAFICO kama shirika la kimkakati hasa katika dhana ya kutekeleza uchumi wa blue.

"Shirika linajukumu la kuwasaidia wavuvii wadogo wadogo hasa katika kunyanyua vipato vyao, kuwawezesha kuhifadhi mazao yao ya uvuvi kuingia ubia na wananchi mbalimbali katika shughuli za uvuvi bahari kuu"



WFP yakabidhi vifaa vya mawasiliano kwa ofisi ya waziri mkuu.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu ) Mhe. Ummy Nderiananga amepokea vifaa vya mawasiliano vitakavyotumika katika kukabiliana na maafa mbalimbali hapa nchini ambavyo ni Ndege zisizo na Rubani (Drones) vyenye thamani ya shilingi Milioni 102,741,400 vilivyotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP)

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo yaliyofanyika katika Ukumbi wa Ofisi hiyo Jijini Dodoma Mhe. Ummy alisema vifaa hivyo vitawezesha Ofisi ya waziri mkuu kutekeleza taarifa katika picha ili kupata majanga na madhara pindi yanapotokea katika nyanja za sekta na taasisi za serikali.

Mhe. Ummy alieleza kwamba vifaa hivyo ni muhimu kwa kuzingatia jukumu kuu la Ofisi ya Waziri Mkuu ambalo ni Uratibu wa shughuli za Serikali na uratibu wa shughuli za maafa na taasisi zisizo za kiserikali kwa njia ya mtandao.

"Kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, tunaishukuru WFP binafsi na shirika la WFP kwa kutupatia vifaa hivi muhimu kwa ajili ya kuimarisha mawasiliano kwa njia ya mtandao, kufanya operesheni za utafutaji na uokoaji, kupata ramani za hatari zilizopo, uwezekano wa kuathiriwa na janga na uwezo wa jamii husika,"Alisema Mhe. Ummy.

Aidha aliishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais, Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kushirikiana na Mashirika mbalimbali ya Umoja wa Mataifa ambayo yamekuwa yakiiunga mkono Serikali katika miradi ya maendeleo kwa manufaa ya wananchi na Taifa.

Awali akimkaribisha Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu ) Mhe. Ummy Nderiananga, Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Dkt. John Jingu alibainisha kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu iko tayari kushirikiana na (WFP) kwa kila eneo ambalo watahitaji ushirikiano huku akiahidi vifaa hivyo kutumika kama ilivyokusudiwa.

"Tunakumbana na maafa mengi na huwa inachukuwa mda mrefu kwa waokozi au upataji wa taarifa unachelewa hivyo,kwaajili ya hizi drone naamini ufanyaji kazi na upatikanaji wa uhalisia wa tukio utapatikana kwa uraisi".

Aidha Mkurugenzi Mkazi Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) Bi. Sarah Gibson alifafanua kuwa mradi huo ni endelevu kwa miaka mitano kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2027 na kwamba Shirika litafanya kazi zake kulingana na viupembeel vya serikali na kuwekeza katika kilimo, elimu, maafa pamoja na wakimbizi.



## Katibu Mkuu Dkt jingu: Zingatieni uzalendo ili tupate Takwimu sahihi

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu Dkt. John Jingu amewaasa makarani wa Sensa ya Watu na Makazi kuwa wazalendo katika zoezi la sensa linalotarajiwa kufanyika tarehe 23 Agosti, 2022 ili kuwa na takwimu sahihi zitakazoleta tija kwa Taifa.

Ametoa kauli hiyo aliwatembelea na kuzungumza na Makarani, Wasimamizi wa Maudhui pamoja na TEHAMA katika Kituo cha Yombo kilichopo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika Wilaya ya Ubungo.

Alisema kuwa, Serikali imewaamini kuwapa jukumu la kukusanya taarifa hizo hivyo hawana budi kuitumia fursa hiyo kwa usahihi kwa kuzingatia weledi na uzalendo wa hali ya juu.

"Takwimu ni jambo muhimu, zoezi hili litasaidia kuwa na taarifa sahihi za takwimu zitakazosaidia shughuli za maendeleo, hata kwa wawekezaji na wafanyabiashara wetu ambao watajua namna bora ya kufanya shughuli zao zitakazochagiza katika ukuaji wa uchumi nchini,"Dkt. Jingu

Aliongezea kuwa Serikali imelipa kipaumbeke suala la sensa hivyo ni wajibu wa kila mmoja kulibeba jambo hilo kwa unyeti wake, maana linategemewa na taifa zima.

Kwa upande wake Msimamizi wa Mafunzo ya Sensa katika kituo hicho Bi. Joyce Zawadi alimpongeza katibu Mkuu huyo kwa kutenga muda na kuwatembelea huku akiahidi kuendelea kusimamia mafunzo hayo kwa weledi ili kufanikisha nia ya Serikali.

“Hatutaliangusha Taifa wala Mhe. Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan tupo tayari kuleta matokeo chanya kwa maendeleo ya nchi yetu,”alisema Joyce




## Idara ya Maafa yawapiga msasa wabunge.

Idara ya Menenjimenti ya Maafa imefanya semina ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Usimaizi wa Maafa ili kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu sheria na namna zinavyofanya kazi pindi maafa yanapojitokeza.

Semina hiyo ilifanyika katika Ukumbi wa Bunge Jijini Dodoma ikihusisha wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria iliyoandaliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Idara ya Menejimenti ya Maafa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu imepewa jukumu la kuratibu na kushughulikia maafa na dharura zote ikijumuisha shughuli za Kuzuia, Kujiandaa, Kukabili na Kurejesha hali.

Viilevile Shughuli za kila siku za Idara zinaongozwa na Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Maafa ya mwaka 2004 na sheria ya Menejimenti ya Maafa Na.7 ya mwaka 2015.

KATIBU MKUU
Ofisi ya Waziri Mkuu
2 Mtaa wa Relini, S. L.P 980
40480 Dodoma,
Barua pepe;ps@pmo.go.tz, Simu;+255262322480
Fax:+255262324534, Tovuti: www.pmo.go.tz